BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya
Chukwani,Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

**HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA MAHAKAMA YA KADHI NAM. 9 YA 2017 NA KUTUNGA SHERIA YA MAHAKAMA ZA KADHI NA KUWEKA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO.**

**Mheshimiwa Spika,** sifa njema zote zinamstahikia Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehma, Mwenye kurehemu ambaye ameumba mbingu na ardhi pamoja na vilivyomo ndani yake na kuviwekea taratibu ili zifuatwe. Pia, tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na afya njema ambayo imetuwezesha kwa mara nyengine kukutana tena siku ya leo katika Baraza hili kwa lengo la kutekeleza majukumu yetu kwa salama na amani.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa mbele ya Baraza lako Tukufu katika kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Mahakama ya Kadhi Nam. 9 ya 2017 na Kutunga Sheria ya Mahakama za Kadhi na Kuweka Mambo Mengine yanayohusiana na Hayo. Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu akuzidishie hekima, busara pamoja na afya njema itakayokuwezesha kutekeleza vyema majukumu yako kwa ufanisi na weledi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa nia njema kabisa inampongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa utekelezaji wake mzuri wa majukumu yake ambayo yamepangwa kupitia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya 2020 - 2025, yanayoleta

mabadiliko makubwa katika nyanja zote za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu azidi kumpa uhai na afya njema ili aweze kuitumikia zaidi nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, kamati inatoa pongezi kwa Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora; Mheshimiwa, Mwl. Haroun Ali Suleiman Aidha, pamoja na Watendaji wote wa Ofisi hii wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndg. Mansura M. Kassim kwa kusimamia vyema na kuandika upya sheria hii ambayo inakwenda kuimarisha utendaji kazi wa Mahakama za Kadhi katika ngazi za Awali, Wilaya na Mikoa.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, kamati inawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Mahakama ya Kadhi wakiongozwa na Kadhi Mkuu wa Zanzibar Sheikh Hassan Othman Ngwali na Naibu Kadhi Mkuu Sheikh Othman Ame Chum kwa namna wanavyotekeleza majukumu yao katika kukuza na kuendeleza Mahakama ya Kadhi ili kuwa chombo chenye ufanisi katika utoaji wa haki.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Kamati inawashukuru na kuwapongeza wadau wote walioshiriki kwa niaba ya taasisi zao katika mswada huu kwa ajili ya kutoa maoni yao yenye hekima na kuimarisha misingi ya haki na sharia ya Dini ya Kiislamu. Miongoni mwa washiriki hao ni kutoka Kituo cha Wanavyuoni Zanzibar, Zanzibar University, Umoja wa Kiislamu wa Uchumi, Elimu na Maendeleo (UKUEM), Jumuiya ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA) na Jumuiya ya Wakalimani wa Lugha za Alama (JUWALAZA). Imani yangu kuwa michango yao mizuri waliyoitoa itasaidia sana katika kuufanya Mswada huu kuwa bora zaidi. Kwa mantiki hiyo, napenda kuwahakikishia kwamba maoni na ushauri wao umezingatiwa na Kamati wakati ilipokaa na Wizara ili kupatiwa ufafanuzi kuhusu Mswada huu.

**Mheshimiwa Spika,** sitotenda haki iwapo sitowashukuru Wanasheria kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu pamoja na wataalamu wetu wa Sheria kutoka Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa juhudi zao walizozionesha katika kuwapatia Wajumbe wa Kamati hii maarifa na kutoa ushauri juu ya mambo mbali mbali ambayo misingi yake ni kuufanya

mswada huu kuendana na wakati wa mabadiliko ya kiuchumi na kijamii.

**Mheshimiwa Spika**, pongezi za pekee kwa Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mashirikiano yao makubwa waliyoyatoa na juhudi zao wakati wa kuujadili mswada huu kifungu kwa kifungu ambao matayarisho yake yamefanywa kwa kuzingatia maslahi mapana ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ruhusa yako naomba kuwatambulisha Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Maryam Thani Juma | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Mussa Foum Mussa | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Abdalla Abas Wadi | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Suleiman Haroub Suleiman | Mjumbe |
| *7.* | Mhe. Haji Shaaban Waziri | Mjumbe |
| *8.* | Mhe. Panya Ali Abdalla | Mjumbe |
| *9.* | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu Msaidizi |
| *10.* | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu Msaidizi |
| *11.* | Ndg. Shawana Mohammed Haji | Katibu Msaidizi |
| *12.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani wa Lugha za Alama |

**Mheshimiwa Spika,** naomba uniruhusu nieleze baadhi ya marekebisho na mapendekezo

mbali mbali ambayo Kamati yetu imeyafanya na pia, naomba kuwatanabahisha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu ya kwamba, hotuba hii inatoa ufafanuzi wa baadhi tu ya vifungu ambavyo vimependekezwa na kufanyiwa marekebisho na Kamati, hivyo maelezo zaidi ya mapendekezo hayo yamo katika muhtasari wa marekebisho yetu ambayo Waheshimiwa Wajumbe tayari mmeshawekewa katika vishkwambi vyenu.

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilitaka ufafanuzi katika kifungu cha Pili cha Mswada kilichobeba dhima ya **ufafanuzi** wa maneno ambayo yametumika bila kufuata utaratibu mzuri wa kiuandishi "alphabetical order". Hivyo, Kamati inashauri kuwepo kwa utaratibu mmoja wa kiuandishi uliokubalika kwa miswada yote inaletwa Baraza la Wawakishi ili kuleta usawa wa sheria hizo.

**Mheshimiwa Spika**, sambamba na hilo, kamati inashauri pia katika kifungu hichi cha Matumizi kufanywamarekebisho madogo kwa kufutwa Tafsiri ya neno **"Ulamaa"** yenye maana ya **"mtu yeyote aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 10 cha Sheria hii"** na kuwekwa badala yake tafsiri ya neno hilo kama ilivyoelezwa katika **Sheria ya Mufti Namba 4 ya mwaka 2021** ili kuipa usahihi tafsiri ya neno hilo lilitumika katika Mswada huu.

**Mheshimiwa Spika,** kamati imeridhika na Kifungu cha Kumi cha Mswada huu ambacho kimetoa fursa ya hiari kwa mdaawa Muislamu kufungua shauri lake la sheria ya Kiislamu iwapo hakuridhika na maamuzi yaliyotolewa na Mahakama ya Kadhi ya Rufaa kwenda kuwasilisha Rufaa katika Mahakama Kuu ili kutafuta haki ambayo kimsingi anahisi amenyimwa katika Mahakama ya Rufaa. Hata hivyo, kamati inashauri kwa kuwa uwamuzi wa Mahakama Kuu utakuwa wa mwisho kwa mdaawa ambaye hakuridhika na uamuzi uliotolewa katika Mahakama ya Kadhi ya Rufaa kufuatwa misingi ya dini inayotokana na Mahkama za Kadhi ambako Shauri hilo lilisikilizwa ili kuleta usawa wa uamuzizi utakaotolewa.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha Kumi na Sita cha Mswada huu kamati inapendekeza

kurekebishwa kwa kuongeza aya mpya ya (e) ambayo itabainisha kuwa ***"Kadhi Mkuu au Naibu Kadhi Mkuu awe na umri usiopungua miaka arobaini (40)"*** ili aweze kutimiza matakwa ya nafasi hiyo. Hata hivyo, kamati imeona kigezo cha umri wa miaka 40 kwa Kadhi Mkuu au Naibu Kadhi Mkuu ni kielelezo tosha cha kupata mtu mwenye hekima, busara na uzoefu katika masuala ya Elimu ya Dini ya Kiislamu ambacho pia ni kigezo pekee cha Waislamu katika uongozi kama vile Mtume wetu Muhammad S.A.W. ambaye alipewa utume akiwa na miaka 40. Aidha, kamati inawashauri Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili Tukufu kuunga mkono hoja hii na kuhakikisha sifa za Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu zimewekwa kufuata utaratibu na miongozo ya Uislamu.

**Mheshimiwa Spika,** sehemu ya nne ya Mswada huu imezungumzia Utatuzi wa Migogoro ambayo itaenda kupunguza migogoro kwa Waislamu na jamii kwa ujumla, kwa kufanikisha hilo, Kifungu cha 25 cha Mswada huu kinatoa fursa kwa Mahakama ya Kadhi kuupeleka mgogoro kwenye utatuzi kwa lengo la kutafuta suluhu na kupunguza wingi wa mashauri Mahakamani. Kamati imeona hili ni jambo jema sana na inashauri Kituo cha Mwanakwerekwe kilichoanzishwa kwa lengo la kutoa suluhu ya migogoro kama hiyo kufanya kazi zake kama ilivyokusudiwa. Kamati inashauri kituo kama hiki kuwepo katika Mahakama za Kadhi kwa Mikoa yote ya Unguja na Pemba ili kusaidia kutoa usuluhishi au upatanishi.

**Mheshimiwa Spika,** kamati inatambua umuhimu wa kanuni na miongozo ya kisera iliyomo ndani ya mpango kazi wa Dunia kuhusu watu wenye ulemavu. Aidha, kamati inathamini mchango wanaoutoa katika jamii, ambapo Mahakama za Kadhi pia imetilia mkazo sera hii kwa kuwatambua ndani ya sheria. Kwa maana hiyo, mswada umeweka Kifungu cha 36 ambacho kimeonesha lugha ya kutumika katika Mahakama ili kurahisisha mawasiliano. Hivyo, kamati inashauri katika kifungu kidogo cha (2) kurekebishwa kwa kufutwa maneno **"ulemavu wa kuzungumza"** yaliyopo baina ya neno **"ana"** na neno **"au"** na badala yake kuwekwa neno **"ulemavu wa uziwi"** ili kwenda sambamba na maana halisi iliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** wakati Kamati ikiupitia Mswada huu ilishauri kufanyiwa marekebisho kifungu cha 38 katika kifungu kidogo cha (2) kwa kufutwa maneno **"elimu ya msingi"** liliopo baina ya neno **"na"** na **"ya"** na kuwekwa badala yake maneno **"elimu ya uwelewa"** baada ya kupata ufafanuzi juu ya maana kamili iliyokusudiwa ndani ya elimu ya msingi ambayo **"Vakili"** anatakiwa kuwa nayo ili aweze kuhudhuria kwa niaba ya mdaawa katika Mahakama ya Kadhi au Mahakama Kuu.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuhitimisha hotuba hii kwa kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini wakati wote ambao naiwasilisha hotuba hii. Aidha, Kwa niaba ya Kamati inawaomba wajumbe wa Baraza hili Tukufu kwamba Mswada huu ulio mbele yetu waujadili na wauchangie ipasavyo na hatimae kuupitisha ili kuwa sheria ambayo itawezesha kutekeleza vyema mashauri yote yanafunguliwa katika Mahakama zetu.

**Mheshimiwa Spika, Naomba kuwasilisha**.

Ahsante,



..................................

**(*Maryam Thani Juma*)**

**Kny. Mwenyekiti,**

**Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,**

**BARAZA LA WAWAKILISHI,**

**ZANZIBAR**